

## TAARIFA KWA UMMA



### BODI YA BIMA YA AMANA

#### KATIKA SHAURI LA KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LTD (ILIYO CHINI YA UFILISI)

#### MALIPO YA FIDIA YA AMANA KWA WATEJA WA KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LTD (CHINI YA UFILISI)

Kufuatia uamuzi wa Benki Kuu ya Tanzania kuifutia **KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LTD** leseni ya kufanya shughuli za kibenki mnamo tarehe 4 Januari, 2018, Bodi ya Bima ya Amana inatangaza kuanza kulipa fidia ya bima ya amana kwa wenye amana katika ofisi za **KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LTD** (Iliyo Chini ya Ufilisi) kuanzia Jumatano tarehe 28 Machi, 2018. Fidia hii inalipwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

#### Ili kufanikisha malipo ya fidia hiyo, wenye amana wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

- (a) **Mahali na Muda wa Malipo**  
Malipo ya fidia ya bima ya amana yatafanyika katika ofisi za iliyokuwa **KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LTD** Muda wa saa za kazi utakuwa kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 10.30 jioni katika siku za Jumatatu hadi Ijumaa na kuanzia saa 3.00 asubuhi hadi saa 6.30 mchana kwa siku za Jumamosi.
- (b) **Ukomo wa Malipo ya Fidia**  
Kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, fidia ya bima ya amana ni hadi shilingi 1,500,000/-.
- (c) **Madai kwa amana zinazozidi Shilingi 1,500,000/-**  
Kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, kwa wale wenye amana zinazozidi Shilingi 1,500,000/-, watalipwa kwa mujibu wa utaratibu wa ufilisi kama itakavotangazwa.
- (d) **Viambatanisho vinavyohitajika**
  - (i) **Fomu ya Madai** iliyojazwa vizuri pamoja na nakala yake: Fomu hii inapatikana katika ofisi za iliyokuwa **KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LTD** (Iliyo chini ya ufilisi) na katika tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania: [www.bot.go.tz](http://www.bot.go.tz)
  - (ii) Kadi ya Utambulisho wa Mwenye Akaunti
  - (iii) Utambulisho halisi wa mwenye amana kwa kuonyesha kimoja wapo kati ya; Kitambulisho cha Uraia, Hati ya Kusafiria, na kwa walio Watanzania, wanaweza kuwasilisha Leseni ya Udereva, Barua ya Utambulisho kutoka kwa Mamlaka ya Serikali ya Mtaa/Sheha au kitambulisho cha mpiga kura.

#### Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:

**Mkurugenzi**  
**Bodi ya Bima ya Amana**  
**Mtaa 2 Mirambo**  
**S. L. P 2939**  
**11884 Dar es Salaam**  
**Simu: + 255 22 223 5390**  
Barua pepe: [DIB-INFO@bot.go.tz](mailto:DIB-INFO@bot.go.tz)

**Imetolewa na:**  
**Mkurugenzi, Bodi ya Bima ya Amana**  
Tarehe: 17 Machi, 2018